

# NEWALA FM REDIO S.L.P 16 NEWALA

Kumb Na NFM/F.15/2024



10-02-2024

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mwenyekiti wa Bodi ya wakurugenzi redio newala anapenda kuwatangazia wananchi wenye sifa nafasi za kazi (ajira ya mkataba)

### WATANGAZAJI/WAANDISHI WA HABARI NAFASI- 8

#### Sifa za mwombaji

1. Awe raia wa Tanzania
2. Awe amemaliza kidato cha nne au kidato cha sita
3. Awe amefuzu mafunzo ya uandishi wa habari ngazi ya diploma na kuendelea
4. Awe amesoma chuo chochote kinachotambulika na serikali
5. Awe na uzoefu katika kazi ya utangazaji na uandishi wa habari
6. Awe na uwezo wa kuzungumza lugha ya Kiswahili na kiingereza kwa ufasaha
7. Awe mbunifu kwenye utayarishaji wa vipindi
8. Maombi yote yaambatanishwe na nakala na vyeti vya elimu na taalumu kutoka chuo kinachotambulika na serikali pamoja na maelezo binafsi (CV)

### KAZI NA MAJUKUMU YA MTANGAZAJI NA MWANDISHI WA HABARI

- kuandaa vipindi na kuvitangaza
- kuandaa habari mbalimbali na kuzitangaza
- kubuni na kushauri habari zinazoendana na jamii zenye maslahi kwa taifa letu
- kutafuta habari ndani na nje ya Tanzania

### MSHAHARA

Mshahara- utatokana na makubaliano ya mkataba na mwajiri

### WALINZI NAFASI- 2

#### Sifa za muombaji

1. Awe raia ya Tanzania
2. Awe amemaliza elimu ya msingi au elimu ya sekondari
3. Awe amepitia mafunzo ya Mgambo na kufanikiwa kupata cheti
4. Awe mwaninifu wakati wa kulinda mali za redio
5. Awe na uzoefu wa shughuli za ulinzi

#### kazi na majukumu

1. Kulinda mali zote eneo la ofisi
2. Kutoa taarifa za usalama wa kituo kwa viongozi wa redio
3. Kuhakikisha kunakua na usalama usiku na mchana eneo la ofisi

### MSHAHARA

Mshahara- utatokana na makubaliano ya mkataba na mwajiri

## MUHUDUMU NAFASI- 1

### Sifa za mwombaji

1. Awe raia wa Tanzania
2. Awe amaliza elimu ya sekondari na zaidi
3. Awe mwaminifu wakati wote wa kazi
4. Awe na uwezo wa kutunza siri za ofisi
5. Awe na uwezo mwingine wa ziada wa kutumia computer

### Kazi na majukumu

1. kufanya usafi ndani na nje ya ofisi
2. kuwapokea wageni na kuwahudumia/kuwapeleka sehemu husika na majukumu mengine ya ziada atakayopangiwa na kiongozi

## MSHAHARA

Mshahara- utatokana na makubaliano ya mkataba na mwajiri

## AFISA MASOKO NAFASI -1

### Sifa za mwombaji

1. Awe raia wa Tanzania
2. Awe na elimu ya biashara ngazi ya diploma kutoka chuo chochote kinachotambulika na serikali ambaye amejiumarisha katika fani zifuatazo
  - masoko
  - mipango ya miradi na uongozi katika biashara
3. Awe mwenye kujiamini na mwenye uwezo wa kumshawishi mteja
4. Lazima awe amesoma computer na kuwa na uwezo wa kuitumia ipasavyo
5. Awe na uwezo wa kuzungumza lugha ya kiswahili na kiingereza kwa ufasaha

### Kazi na majukumu

1. kutafuta masoko
2. kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu uboreshaji wa masoko na kuongeza kipato
3. kutangaza ubora wa huduma zinazotolewa kwa wateja ili kuwavutia kwa lengo la kuongeza wigo mapato
4. kuandaa na kutoa taaarifa kwa meneja wa redio kuhusu hali ya masoko
5. kushawishi wateja au makampuni kutumia njia bora ya kitaaluma ili kuongeza wigo la mapato

## MSHAHARA

Mshahara- utatokana na makubaliano ya mkataba na mwajiri

Barua zote zitumwe kwa anuani  
Mwenyekiti wa Bodi ya wakurugenzi Newala FM  
S.L.P 16  
Newala

Au Barua pepe

[newala.radio@newaladc.go.tz](mailto:newala.radio@newaladc.go.tz) au unaweza kufikisha barua yako ofisi za redio newala zilizopo jengo NA. 39 barabara ya newala fm newala mjini Maombi yatapokelewa kuanzia tarehe 12-02-2024 mwisho tarehe 25-02-2024

MWENYEKITI WA BODI YA WAKURUGENZI  
NEWALA FM

